Nia Dhidi Ya Ulimwengu (Attitude Towards the World)

Na

Ellis P. Forsman

Nia Dhidi Ya Ulimwengu

Na

Ellis P. Forsman

Oktoba 6, 2011

Nia Dhidi Ya Ulimwengu

Mat. 16:21-23

Kimsingi nia njema ni muhimu. Ni muhimu katika umoja ndani ya kusanyiko la mahali fulani.

Tulijifunza kuhusu nia yetu dhidi ya Mungu, Yesu Kristo, Injili, Kanisa, ndugu zetu, na sisi wenyewe; sasa tutajifunza kuhusu nia yetu dhidi ya ulimwengu.

Ninapenda kusema tukio lililotokea miaka kadhaa iliyopita.

Katika kampuni ya ndege ya Eastern Airline, ndege 401 ilianguka Florida Disemba 29, 1972, na ilikuwa na abiria 200 ndani. Ujumbe ufuatao ulikusanywa kutoka katika chombo cha kunasia safari za ndege.

Wakati wa kuondoka mwanga mdogo ulionekana (tairi ya mbele) ilitoka. Injinia wa ndege akaiona na kuanza kuuliza maswali. Kwa vile kila kitu kilikuwa sawa, akafikia maamuzi kwamba ni glopu iliyoungua. Hivyo akaamua kuitoa na kuweka nyingine.

Akiwa na shida kidogo akamuuliza rubani msaidizi ili aweze kumsaidia. Rubani huyo akaairisha kutua, akaileta ndege hadi hatua 2000, na kuanza kuzunguka hadi wakaimaliza tatizo. Wawili hao wakiwa wanafanya kazi pamoja walishindwa kubadilisha ile glopu, hivyo rubani akaiweka ndege katika hali ya kawaida na kuja kusaidia. Kila mmoja wao alikuwa na wazo tofauti kuhusu jinsi ya kuondoa tatizo na mazungumzo ya ukali yakaanza miongoni mwao. Walipaswa tu kurekebisha tatizo.

Vile vile, ndege ile ilikuwa inashuka. Mtazamo wa muongoza ndege ulikuwa katika glopu ya bei ya juu, wakati ndege ni ya gharama na watu 200 wakiangamia ardhini na kufa wote.

Petro, vile vile, alikuwa na tatizo la kuwa na hasira. Mat. 16:21-23, "*Tangu wakati huo Yesu alianza kuwaonya wanafunzi wake ya kwamba imempasa kwenda Yerusalemu, na kupata mateso mengi kwa wakuu wa makuhani, na waandishi na kuuawa, na siku ya tatu kufufuka. Petro akamchukua akaanza kumkemea, akisema hasha Bwana, hayo hayatakupata. Akageuka akamwambia Petro, nenda nyuma yangu shetani, u kikwazo kwangu maana huyawazi yaliyo ya Mungu, bali ya wanadamu.*"

Je! Si ungechukia Mwana wa Mungu akikwambia kwamba Shetani yu ndani yako?

Lakini mtazamo wa Petro ulikuwa wa kibinafsi na kupotea.

2 Tim. 2:4, "*Hakuna apigaye vita ajitiaye katika shughuli za dunia ili ampendeze yeye aliyemwandika awe askari.*"

Tuko katika Jukumu Gani?

Miaka iliyopita Ndg. Howard McCay alikuwa kazini katika chuo huko Yakima, na akasikia mkuu wake akimpia kelele mfanyakazi mwenzake, "Kipi katika ulimwengu unachokifanya, kwa ajili ya mbingu!" Ndg. Howard akatengeneza somo juu ya kichwa hiki: "Nini katika ulimwengu unachofanya kwa ajili ya mbingu!

Huu ndio mlolongo wetu! Huu ndio biashara yetu!

- Mat. 28:19-20, "*Basi enendeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama mimi nipo pamoja nanyi siku zote hata ukamilifu wa dahari.*"
- Marko 16:15-16, "*Akawaambia enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini, atahukumiwa.*"

Tumeagizwa na Bwana wetu kwenda katika ulimwengu na kuwafanya Wakristo wenzetu.

Sababu za Kufanya Uinjilisti

Kufuata mfano wa Kristo. Luka 19:10, "*Kwa kuwa Mwana wa Adamu alikuja kutafuta na kuokoa kile kilichopotea.*"

Kristo hakuja kusuhisha matatizo ya kisiasa ya Israeli, au kuvunja ukuta wa Rumi, au kuleta maendeleo katika kilimo, au elimu, au tatizo lolote linalofanana na hayo. Bali alikuja kuwakomboa wanadamu kutoka dhambini.

Yohana 3:16-17, "*Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe pekee ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele. Maana Mungu hakumtuma Mwana ulimwenguni ili auhukumu ulimwengu, bali ulimwengu uokolewe katika yeye.*"

Paulo akasema katika 1 Tim. 1:15, "*Ni neno la kuaminiwa tena lastahili kukubalika kabisa, ya kwamba Kristo Yesu alikuja ulimwenguni awaokoe wenye dhambi; ambao wa kwanza wao ni mimi.*"

Hakika Paulo alikuwa anatoa shukrani kwamba Kristo alimuokoa. Yohana 20:21, "*Basi Yesu akawaambia tena, amani iwe kwenu; kama Baba alivyonituma mimi, mimi name nawapeleka ninyi.*"

Sisi pia tumeagizwa kwenda.

Tunataka kuzingatia kwamba Yesu alishughulikia watu ana kwa ana. Alimwambia Nikodemo. Yohana 3:3, "*…mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuuona ufalme wa Mungu.*"

Alimfundisha mwanamke kisimani. Yohana 4:25-26, "*Yule mwanamke akamwambia najua ya kuwa yuaja Masihi aitwaye Kristo; naye atakapokuja atatufunulia mambo yote. Yesu akamwambia, mimi ninayesema nawe, ndiye.*"

Alikaribishwa katika nyumba ya Zakayo. Luka 19:5, "*Na Yesu alipofika mahali pale, alitazama juu akamwambia Zakayo, shuka upesi kwa kuwa leo imenipasa kushinda nyumbani mwako.*"

Unaweza kudhani kwamba hiyo ilikuwa ni upole. Wakatifulani tunapaswa kuwa wapole.

Mungu alikuwa tu na Mwana pekee na alikuwa mhubiri na mwalimu. Tuweza kufanya uinjilisti katika kiwango cha binafsi pia. Sio mafundisho yote yanapaswa kufanywa katika mimbari.

Unjilisti ni Muhimu

Nafsi ambazo hazisikii na kutii injili hazitaokolewa.

2 Tim. 1:7-9, "*Maana Mungu hakutupa roho ya woga, bali ya nguvu na ya upendo na ya moyo wa kiasi. Basi usiuonee haya ushuhuda wa Bwana wetu, wala usinionee haya mimi mfungwa wake, bali uvumilie mabaya pamoja nami kwa ajili ya injili kwa kadiri ya nguvu ya Mungu.*"

Ndugu na dada, swala la kupote kwa nafsi ni mbaya sana. Ni sehemu ya mateso (maumivu, kilio, na kusaga meno). Ni sehemu iliyojaa giza. Ni milele. Mat. 25:46, "*Na hao watakwenda zao kuingia katika adhabu ya milele; bali wenye haki watakwenda katika uzima wa milele.*"

Katika kila dakika nafsi zinakufa – je tunazisikia? Yesu aliona umuhimu wa haraka wa kuwaokoa wenye dhambi. Alikufa kwa ajili yao.

Paulo pia aliona umuhimu. Kol. 1:28, "*Ambaye sisi tunamhubiri habari zake tukimwonya kila mtu, na kumfundisha kila mtu kwa hekima yote tupate kumleta kila mtu mtimilifu katika Kristo.*"

Yesu anaujumbe kwetu sisi pia.

Nafsi ambazo hazileti ujumbe zitapotea pia.

- Ezek.3:16-20, "*Hata ikawa mwisho wa siku saba, neno la BWANA likanijia, kusema, mwanadamu nimekuweka kuwa mlinzi wa nyumba ya Israeli; basi sikia neno hili litokalo katika kinywa change, ukawape maonyo hayo yatokayo kwangu. Nimwambiapo mtu mbaya, hakika utakufa, wewe usimpe*

maonyo, wala husemi na huyo mtu mbaya ili kumwonya, kusudi aache njia yake mbaya na kujiokoa roho yake; mtu yule mbaya atakufa katika uovu wake; lakini damu yake nitaitaka mkononi mwako. Lakini ukimwonya mtu mbaya, wala yeye hauachi ubaya wake, wala njia yake mbaya, atakufa katika uovu wake; bali wewe umejikoa roho yako. Tena mtu mwenye haki aiachapo haki yake na kutenda uovu name nikiweka kikwazo mbele yake, atakufa kwa sababu hukumwonya, atakufa katika uovu wake, wala matendo yake ya haki aliyoyatenda hayatakumbukwa; lakini damu yake nitaitaka mkononi mwako."

- Yakobo 4:17, "*Basi yeye ajuaye kutenda mema wala hayatendi kwake huyo ni dhambi.*"

Hivyo, siyo tu kwamba injili inaokoa mwenye dhambi bali pia mpeleka injili pia.

Fanya Uinjilist Ili Kukidhi Hitaji La Ulimwengu

Kuna baadhi ya watu wanaodhani kwamba kila mtu ataokolewa. Ni huzuni iliyoje jinsi walivyokosea na mshutuko ulioje watakaoupata! Mat. 7:13-14, "*Ingieni kwa kupitia mlango uliomwembamba, maana mlango ni mpana na njia ni pana iendayo upotevuni nao ni wengi waingiao kwa mlango huo. Bali mlango ni mwembamba na njia imesonga iendayo uzimani nao waionao ni wachache.*"

Jehanamu siyo somo maarufu Marekani leo, lakini hatuwezi kuukimbia ukweli wake – kuikataa hakutaifanya iende mbali! Mara nyingi Yesu alizungumzia jehanamu na akawaonya watu juu ya hatari ya kwenda pale.

Mtu anaweza kusema haipendezi kuongelea jehanamu, bali upendo onyo la hatari – kisichopenda ni kujua hatari na kukaa kimya.

Ufu. 20:15, "*Na iwapo mtu yeyote hakuonekana ameandikwa katika kitabu cha uzima, alitupwa katika lile ziwa la moto.*" Hiyo ndio hatari kubwa ninayofikiria.

Yesu aliulilia Yerusalemu, kwa sababu watu hawakumkubali. Mat. 23: 37-38, "*Ee Yerusalemu, Yerusalemu, uwauaye manabii na kuwapiga kwa mawe wale waliotumwa kwako! Ni mara ngapi nimetaka kuwakusanya pamoja watoto wako, kama vile kuku avikusanyavyo pamoja vifaranga vyake chini ya mabawa yake,*

lakini hamkutaka! Angalieni nyumba yenu mmeachiwa hali ya ukiwa."

Paulo aliumia juu ya wa Athene. Mdo. 17:16, "*Paulo alipokuwa akiwangojea huko Athene na kuona jinsi mji ule ulivyojaa sanamu, roho yake ilichukizwa sana ndani yake.*"

Kujali kwetu na huzuni yetu iko wapi kwa waliopotea? Watu bila Mungu wamepotea, hawana msaada, na kuchanganyikiwa. Hawana tumaini na vibaya zaidi wamepotea katika dhambi.

Dhambi hutenganisha nchi yetu na majirani zetu. Huaribu miji na uhai na kufanya maisha kuwa mabaya zaidi. Damu ya Yesu na injili ndio suluhisho letu!

- Mdo. 2:40, "*Akawashuhudia kwa maneno mengine mengi sana na kuwaonya akisema jiokoeni na kizazi hiki chenye ukaidi.*"
- Gal. 1:4, "*Ambaye alijitoa nafsi yake kwa ajili ya dhambi zetu, ili atuokoe na dunia hii mbovu iliyopo sasa kama alivyopenda Mungu Baba yetu.*"

Tusiratajie mtu ye yote kupatwa na tatizo katika maisha haya. Kama ilikuwa ndani ya uwezo wetu, tunapaswa kufanya kila tuwezalo ili kumuepusha katika…

- Kupoteza mguu, jicho.
- Kupoteza kazi.
- Kupoteza nyumba.
- Kuwapoteza wapendwa wao.

Kuka milele katika jehanamu ni mbaya kuliko mambo haya yote. Tunapaswa kutafuta na kuokoa kilichopotea, kama Bwana wetu alivyofanya.

Uinjilisti Umeagizwa

Kusudi la Yesu kuja ulimwenguni na kufa lilikuwa ni kuwaokoa wenye dhambi. 1 Tim. 1:15, "*Ni neno la kuaminiwa tena lastahili kukubalika kabisa ya kwamba Kristo Yesu alikuja ulimwenguni awaokoe wenye dhambi, ambao wa kwanza wao ni mimi.*"

Wote ambao Mungu amewaokoa wameagizwa kuhubiri na kufundisha. Marko 16:15-16, "*Akawaambia enendeni ulimwenguni mwote mkaihubiri injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokoa, asiyeamini atahukumiwa.*"

Paulo alielewa kwamba injili ili iwe injili ni lazima iwe injili ya upatanisho (wenye dhambi wapatanishwe na Mungu). 2 Kor. 5:18-19, "*Lakini vyote pia vyatokana na Mungu, aliyetupatanisha sisi na nafsi yake kwa Kristo, naye alitupa huduma ya upatanisho; yaani Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake, asiwahesabie makosa yao; naye ametia ndani yetu neno la upatanisho.*"

Kanisa la kwanza lilitilia maanani agizo la Bwana. Mdo. 8:4, "*Lakini wale waliotawanyika wakaenda huko na huko wakilihubiri neno.*"

Na sisi pia tunapaswa kulitilia agizo lake maanani.

Unjilisti unatufanya kuwa wafanyakazi wenza wa Mungu

2 Kor. 6:1, "*Nasi tukitenda kazi pamoja naye twawasihi msiipokee neema ya Mungu bure.*"

Anatutumia kuisambaza injili yake. 2 Kor. 4:7, "*Lakini tunahazina hii katika vyombo vya udongo, ili adhama kuu ya uwezo iwe ya Mungu, wala si kutoka kwetu.*"

Ni heshima kuu kufanya kazi na Mungu katika juhudi hizi kuu. Tunapomfanyia kazi naye anatufanyia.

Je, unajisikia vizuri kufanya kazi na Mungu? Au je umewahi kuifikiria? Ni kitu ambacho tunapaswa kufurahi kuifanya daima.

Uinjilisti Unafanya Kazi Katika Sheria ya Kupanda na Kuvuna

Gal. 6:7, "*Msidanganyike Mungu hadhihakiwi, kwa kuwa cho chote apandacho mtu ndicho atakachovuna.*"

Neno ndiyo mbegu. Luka 8:11, "*Na huo mfano maana yake ni hii; mbegu ni neno la Mungu.*" Mbegu hiyo lazima ipandikizwe kwa sababu kutakuwa na mavuno.

Mifano kutoka katika Matendo ya Mitume.

- Walizidishwa watu 3,000. Mdo. 2:41, "*Nao waliolipokea neno lake wakabatizwa, na siku ile wakaongezeka watu wapata elfu tatu.*"
- Watu 5,000. Mdo. 4:4, "*Lakini wengi katika hao waliolisikia lile neno waliamini na hesabu ya watu waume ikawa kama elfu tano.*"

- Watu wengi. Mdo. 5:14, "*Walioamini wakazidi kuongezeka kwa Bwana, wengi waume na wanawake.*"

Tusipofanya uinjilisti (kufundisha neno kwa waliopotea), wengi watakufa ambao tungesaidia

Fanya Uinjilisti Kutimiza Kusudi Letu La Ndani

Wazee wa Makuhani walipowaamuru mitume kuacha kuhubiri katika jina la Yesu, mitume wakasema katika: Mdo. 4: 19-20, "*Petro na Yohana wakajibu wakawaambia, kwamba ni haki mbele za Mungu kuwasikiliza ninyi kuliko Mungu, hukumuni ninyi wenyewe, maana sisi hatuwezi kuacha kuyanena mambo tuliyoyaona na kuyasikia.*"

- Ni sawa na mwanamke aliyevalishwa pete ya uchumba, ni vigumu kukaa kimya.
- Ni sawa na binti mdogo anayetarajia mtoto.
- Ni habari njema tulionayo kwa waliopotea.

2 Kor. 5:14-15, "*Maana upendo wa Kristo watubidisha, maana tumehukumiwa hivi ya kwamba mmoja alikufa kwa ajili ya wote, basi walikufa wote; tena alikufa kwa ajili ya wote, ili walio hai wasiwe hai tena kwa ajili ya nafsi zao wenyewe, bali kwa ajili yake yeye aliyekufa akafufuka kwa ajili yao.*"

Tunapofanyika Wakristo tunaishi kwa Kristo. Rum. 1:14-16, "*Nawiwa na Wayunani na wasio Wayunani, nawiwa na wenye hekima na wasio na hekima. Kwa hiyo kwa upande wangu mimi ni tayari kuihubiri Injili hata na kwenu ninyi mkaao Rumi. Kwa maana siionei haya Injili, kwa sababu ni uweza wa Mungu uuletao wokovu kwa kila aaminiye, kwa Myahudi kwanza na kwa Myunani pia.*"

Paulo alisema.

- Niko chini ya jukumu.
- Nina shauku.
- Sioni haya.

Mdo. 20:24, "*Lakini siyahesabu maisha yangu kuwa kitu cha thamani kwangu kama kuumaliza mwendo wangu na huduma ile niliyopokea kwa Bwana Yesu, kuishuhudia habari njema ya neema ya Mungu.*"

Paulo anaonyesha kwamba huduma yake kwa Mungu ni muhimu sana kuliko maisha yake mwenyewe. Je, unania kama hiyo?

Kuwafanya Wanafunzi

Siyo tu kwamba Mungu anatutaka kufundisha na kutoka nje, anataka wanafunzi.

Wanafunzi ni wale wanaomfuata Yesu na kuvutiwa kuwafundisha wengine wafanye hivyo.

Je, wewe ni mwanafunzi? Mkomavu, muwajibikaji, anayezaa wafuasi!

Kama ungekuwa na rafiki anataka kufanyika Mkristo, waweza kumfundisha? 2 Tim.2:2, "*Na mambo yale uliyoyasikia kwangu mbele ya mashahidi wengi, hayo uwakabidhi watu waaminifu watakaofaa kuwafundisha wengine.*"

Kuwa tayari siku zote kutoa jibu

1 Pet. 3:15, "*Mwe tayari siku zote kumjibu kila mtu awaulizaye habari za tumaini lililo ndani yenu; lakini kwa upole na hofu.*"

Kufanya hivi lazima tujifunze. 2 Tim. 2:15, "*Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali neno la kweli.*"

Nia yetu ni kama ile ya kijana tajiri? Je, tunataka kumtumikia Yesu, na hatujajitokeza nje kwa ajili yake.

Masaa mengi yametumika katika ulimwengu huu uliozeeka tukijiandaa kwa ajili ya maisha mazuri. Vipi kuhusu maisha yetu ya Ukristo?

Mdo. 17:11, "*Watu hawa walikuwa waungwana kuliko wale wa Thesalonike, kwa kuwa walilipokea lile neno kwa uelekevu wa moyo, wakayachunguza maandiko kila siku waone kwamba mambo hayo ndivyo yalivyo.*"

Nia njema ni nzuri. Sikiliza nia zinavyoelezewa katika vifungu vifuatavyo.

- 1 Pet. 3:15, "*Mwe tayari siku zote kumjibu kila mtu awaulizaye habari za tumaini lililo ndani yenu; lakini kwa upole na kwa hofu.*"
- Kol. 4:6, "*Maneno yenu yawe na neema siku zote, yakikolea munyu, mpate kujua jinsi iwapasavyo kumjibu kila mtu.*"

- 2 Tim. 2:25, "*Akiwaonya kwa upole wao washindanao naye, ili kama ikiwezekana, Mungu awape kutubu na kuijua kweli;*"

Hitimisho

Je, Yesu anaweza kukuhesabu?

Nia yako ni ipi katika kuihubiria ulimwengu?

Je, kizazi kijacho kitaijua kweli? Watoto wetu watamfuata Yesu?

Majirani zetu watafahamu kwamba tunampenda Bwana na kumtumikia?

Utakuwa na muda kwa ajili ya Bwana?

Utakwenda mbinguni ukifa?